

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kuna maeneo ya Mila, Desturi, Historia na Kiutamaduni ambavyo ni vivutio vyta kitalii.

- ❖ Kuna Eneo la “ kisima cha Dodoma” kipo kitongoji cha Bwenda kata ya Katente kisima hicho ni cha asili hakikauki maji hata utokee Ukame na kimekuwepo tangu zama za kale na ukivua samaki katika kisima hicho wakipikwa hawaiivi,na masharti ya kuingia katika kisima hicho ni lazima uvue viatu pia samaki hao huonekana kwa majira tofauti.



Kisima kisichokauka maji na ukivua samaki katika kisima hiki hawapikiki (Hawaivi).

❖ Pia katika cha kijiji cha Bwenda kuna eneo maalum kwaajili ya “Kuzika Watemi wa khabila la kisumbwa ambapo mila na desturi za khabila hili watemi hao walikua wanazikwa wakiwa wamekaa,kwa wasumbwa wenyewe hauruhusiwi kuingia maana wanaamini ukingia kwenye eneo la makaburi waliozikwa watemi hao wataitwa kwa njia ya kifo na ndugu zao (ambao ni watemi) hivyo ni mwiko kwa ambaye si msaidizi wa mtemi wakati wa kuzika na hata kwenda kujengea makaburi ,Mtemi huzikwa na wasaidizi wake tu. Aidha eneo hilo la Makaburi ya Watemi hulindwa na wanyama aina ya “Tumbili” na wanyama wengine ambao kwa maelezo ya Wazee wa kisumbwa wanaotoka katika ukoo wa kitemi wanasema “Nyoka wa Mizimu”, na kabla ya kwenda kutembelea eneo hilo ni lazima upate ruhusa ya Mtemi anayetawala sasa akupe baraka zake ndo ufile katika eneo hilo la mila na desturi la khabila ya “Kisumbwa” kinyume na hapo ukienda bila kupitia kwa Mtemi huyo unapotea (umauti unakufika).



Alama inayoonyesha njia ya kwenda kwenye Makaburi ya "Watemi".

Eneo la makaburi ya watemi wa kabilia la Kisumbwa.



Katika ya Eneo la kuingilia kwenye makaburi ya Watemi wa Kisumbwa.

❖ Kuna “Mti wa Maajabu” ambao ukichuma majani yake unakufa upo kata ya Runzewe Mashariki kijiji cha Musasa, chanzo cha kuwepo mti huo ni ukame ulikuwa katika eneo hilo enzi za zamani ndipo Mtemi wa eneo Bwana. Luwasa alipohamua kufunga safari kwenda Kigoma kutafuta dawa ya kuwanusuru wananchi wake na ukame huo uliokuwa umekithiri katika himaya yake alipofika Kigoma akakutana na Mtemi wa huko ndipo alipompatia dawa ya “Mti huo wa maajabu” kwa masharti upandwe kwenye kichunguu na pia majani yoyote ya mti huo yasichumwe sababu yatakapochumwa au kukatwa ndipo Ukame utarudi tena hivyo bada ya Mtemi aliyasadidhia wananchi wake kupata “chemchem” ya maji yasiyokauka hata ukame upi utokee kisima hicho lazima kiwe na maji alipofariki alimrithisha Utemi mjukuu wake Ndugu. Allan Luwasa ambae anafanya matambiko mbalimbali ili kuendelea kulinda kisima hicho cha Maajabu, serikali ilijaribu kujengea, na kuweka bomba kisima hicho lakini kilihama na kwenda eneo jingine la pemberi yake hivyo kutoendeleza kujengea tena isipokuwa kuacha “kisima hicho chenye mti wa ajabu” kubaki na asili yake na hakika ukikata magome ya mti huu wa ajabu au kuchuma jani lolote kutoka kwenye mti huo Unakufa .

‘



Kisima katika mti wa maajabu Serikali ilijengea lakini baada ya kujengewa maji ya kahama na kuhamia eneo linguine la pembeni ambalo halijajengewa.



Mti wenywe wa maajabu na majani ambayo mtu yoyote haruhusiwi kuchuma au kukata magome ambapo ukifanya hivyo Unakufa.



Haya ndiyo Majani ambayo mtu yoyote akichuma anakufa sababu kama wangeruhusu majani yachumwe na magome yakatwe Ukame ungetokea.



Wananchi wakinufaika na uwepo wa kisima hicho kilichotokana na “Mti wa maajabu”.



Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Musasa akichota maji katika kisima hicho ili kutii Kiu yake.



Mwanafunzi huyo akitii kiu yake ya maji kutoka katika  
Mti wa maajabu ulioleta maji.

Wanyama nao wananaufika na uwepo wa maji hayo  
yaliyotokana na mti wa maajabu.





Mjukuu wa Mtemi ambaye amerithishwa utemi na  
babu yake . Mtemi Allan Luwasa wa Runzewe.



Wananchi wanaoishi katika kijiji hiki chenye Mti wa Maajabu unaowaletea maji wakichota maji hayo.

## **Hitimisho.**

Haya ndio maeneo yenye Mila na desturi na ya historia katika Wilaya ya Bukombe, maeneo haya yanaweza kuendelezwa ili kudumisha mila na desuri zetu na kurithisha vizazi vijavyo kufahamu na kuenzi mila na desturi za makabila yao, maana kuna mila na desturi nyingine zilikua zinaokoa maafa makubwa kwasababu Watemi walikuwa wanaomba/kufanya matambiko kwa kuheshimu na kuamini wanachoomba ndiyo maana majanga yalikua hayakabili sana jamii.